TANGAZO LA SERIKALI NA. 204 la Tarehe 15/3/2019

# SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA. 290)

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

## SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA ZA MWAKA 2019

## SEHEMU YA I

## UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya za Mwaka 2019 na zitaanza kutumika rasmi baada ya kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi.

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo cha moto au chombo chochote kinachotumika kusafirishia bidhaa, abiria au mizigo.

"gulio" maana yake ni soko la wazi linalofanyika kwa wakati na siku maalum kwa kibali maalum cha

Halmashauri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Mkurugenzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"kituo cha Mabasi'' maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kushusha abiria au mizigo ya abiria;

"kituo cha mizigo" maana yake ni kituo maalum cha kushusha au kupakia mizigo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"maegesho" maana yake ni sehemu iliyoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanayama na kuanika ngozi;

"madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, kokoto, chokaa, jasi, mawe na matofali yanayopatikana katika eneo la Halmashauri;

"mnada" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza au kununua bidhaa;

"ushuru" maana yake ni malipo ya fedha taslimu zinazolipwa na mtu anayehitaji huduma;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, Kampuni au Shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA II

## NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Utozaji Wa Ada na Ushuru

4. -(1) Halmashauri itatoza Ada na ushuru kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

(2) Ada itozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kabla ya kibali au leseni kutolewa.

(3) Ada na ushuru utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma au kibali husika.

Wajibu wa Kulipa ada na ushuru

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa Ada na Ushuru utozwao kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi, kulipa ada na ushuru kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Ada na Ushuru Kulipwa kwa Halmashauri

6. -(1) Ada inayotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kwa Halmashauri na kutolewa stakabadhi ya kielektoniki kama kielelezo cha kupokea malipo hayo.

(2) Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kwa Halmashauri au Wakala au Afisa Mwidhiniwa

(3) Wakala aliyeteuliwa atawajibika kuzingatia masharti na maelekezo yaliyomo katika Sheria Ndogo hizi pamoja na sheria nyingine.

Muda wa malipo ya Ada na Ushuru

7. (1) Malipo yote ya ada yatalipwa katika Ofisi ya Halmashauri kabla ya kutoa au kupokea kibali au leseni.

(2) Malipo yote ya ushuru yatalipwa kwa wakala au Afisa mwidhiniwa au Ofisi za Halmashauri.

Vibali

8. Kutakuwa na vibali mbalimbali vitakavyotolewa na Halmashauri na kulipiwa Ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Mamlaka ya kuingia katika Jengo

9. Afisa Mwidhiniwa au Wakala kwa idhini ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi anaweza kuingia katika Jengo lolote kwa nia ya kutoza na kukusanya Ushuru.

Uteuzi wa Wakala

10. -(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi kukusanya Ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) atawajibika kukusanya Ushuru kwa kutumia Stakabadhi za Halmashauri

Makosa

11. -(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo :-
   (a) atakataa au atashindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Mwidhiniwa;
   (b) atakataa au atajaribu kukataa kulipa Ushuru anaopaswa kulipa;
   (c) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe ushuru;
   (d) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi Shilingi Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

13. Bila kuathiri kifungu cha 12 hapo juu, Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote anayedaiwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi ikiwa mdaiwa huyo amekiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na kuahidi kuwa atalipa deni analodaiwa pamoja na faini ya isiyopungua shilingi (laki mbili) au isiyozidi shilingi Laki tano.

Kufutwa Tangazo Na.408/2012

14. Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya za Mwaka 2012, zimefutwa na Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa Tangazo Na.407/2012

15. Sheria Ndogo za (Ada za Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya za Mwaka 2012, zimefutwa na Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limeundwa chini ya kifungu cha 5)*

I. ADA YA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

| Na. | Huduma | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya mikutano au vikao au sherehe | Kwa mujibu mkataba |
| 2 | Kukodi viti | Kwa mujibu mkataba |
| 3 | Kukodi Gari au<br>Kukodi trekta | Kwa mujibu mkataba |
| 4 | Vibanda vya biashara mzunguko wa Stendi | Kwa mujibu mkataba |
| 5 | Vibanda vya biashara sokoni | Kwa mujibu mkataba |
| 6 | Kokodi shamba la Halmashauri/kijiji | Kwa mujibu mkataba |
| 7 | Mali nyingine za Halmashauri | Kwa mujibu mkataba |

II. USHURU WA MAZAO YA CHAKULA NA BIASHARA

| *Na.* | *Zao* | *Kiwango/USHURU* |
|---|---|---|
| 1 | Viazi vitamu | 3%ya Bei ya soko |
| 2 | Vitunguu maji | 3%ya Bei ya soko |
| 3 | Matunda | 3%ya Bei ya soko |
| 4 | Karoti | 3%ya Bei ya soko |
| 5 | Kabichi | 3%ya Bei ya soko |
| 6 | Nyanya | 3%ya Bei ya soko |
| 7 | Maharage | 3%ya Bei ya soko |
| 8 | Karanga | 3%ya Bei ya soko |
| 9 | Mchele | 3%ya Bei ya soko |
| 10 | Mazao ya Mboga Mboga | 3%ya Bei ya soko |
| 11 | Viazi mviringo | 3%ya Bei ya soko |
| 12 | Mahindi | 3%ya Bei ya soko |
| 13 | Uwele | 3%ya Bei ya soko |
| 14 | Mtama | 3%ya Bei ya soko |
| 15 | Mpunga | 3%ya Bei ya soko |
| 16 | Mhogo | 3%ya Bei ya soko |
| 17 | Mazao ya matunda | 3%ya Bei ya soko |

III. ADA NA USHURU MAZAO YA BIASHARA

| | | |
|---|---|---|
| 18 | Kahawa | 3%ya Bei ya soko |
| 19 | Pareto | 3%ya bei ya soko |
| 20 | Vitunguu saumu | 3%ya bei ya soko |
| 21 | Ufuta | 3%ya bei ya soko |
| 22 | Alizeti | 3%ya bei ya soko |
| 23 | Mazao mengine | 3%ya bei ya soko |

IV. ADA YA HUDUMA ZA CHANJO,CHAPA, JOSHO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA

| *Na* | *Ada/ushuru* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya Ukaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe atakayechinjwa | 5,000/= kila mmoja |
| 2 | Ada ya Ukaguzi wa nyama kwa kila Kondoo, Mbuzi au Nguruwe atakayechinjwa | 1,000/= kila mmoja |
| 3 | Kuwamba na kukausha ngozi | |
| | (a) Ng'ombe | 1,000/= kila ngozi |
| | (b) Mbuzi, Kondoo au mnyama mwingine | 500/= kwa ngozi |
| 4 | Ushuru wa wachoma nyama. | 2,000/= kwa siku |
| 5 | Ada ya uogeshaji mifugo (Josho) | 500/= kwa ng`ombe |
| 6 | Kibali cha machinjio binafsi | 30,000/= kwa mwaka |
| 7 | Ada ya kusafirisha ngozi | |
| | (a) Ng'ombe | 1,000/= kwa ngozi |
| | (b) Mbuzi, Kondoo au mnyama mwingine | 500/= kwa ngozi |
| 8 | Ada ya chapa ya mifugo. | 1,000 /= kwa mfugo |
| | Ada ya chanjo ya mifugo | inategemea bei ya chanjo |

V. USHURU WA MAUZO YA MIFUGO MINADANI

| *Na* | *Aina ya Mnyama* | *Tozo* |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 5,000/= kwa ng'ombe |
| 2 | Mbuzi | 1,500/= kwa mbuzi |
| 3 | Kondoo | 1,5000/= kwa kondoo |
| 4 | Kuku | 2,000/= kwa tenga |
| 5. | Nguruwe | 1,500/= kwa nguruwe |
| 6. | Wanyama Wengine | 1,500/= kila mnyama |

VI. ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, NA MICHEZO

| *Na* | *A. Ada/Ushuru* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1 | Leseni ya vibanda vya picha jongevu | 60,000/= kwa mwaka |
| 2 | Ada ya kumbi zinapotumik(kumbi) kubwa | 50,000/= kwa tukio |
| 3 | Ada ya kumbi ndogo | 30,000/=kwa tukio |
| 4 | Usajili vyama vya michezo | 10,000/= kwa usajili. |
| 5 | Usajili wa vikundi vya sanaa | 25% ya usajili. |
| 6 | Usajili wa vyama na vilabu vya michezo | 50,000/= kwa usajili |
| 7 | Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho (Sinema, video, maigizo, sarakasi, ada nyingine | 50,000/= Kwa tukio |
| 8 | Kibali cha kuchezesha Michezo ya Kubahatisha kwa kutimia mashine. | 200,000/= Kwa kibali kwa mwaka |
| 9 | Kibali cha mchezo wa pool table | 50,000/=kwa mwaka. |
| 10 | Kibali cha tamasha/kongamano | 20,000/= kwa onesho |
| 11 | Bahati nasibu ndogo ndogo (fete) | 50,000/= kwa kibali |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Kibali cha matangazo | 50,000/= kwa tangazo ya biashara. |

VII. USHURU WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA

A. MAGARI YA MIZIGO

| Aina ya Gari | USHURU | | |
|---|---|---|---|
| | Kwa Saa | Kwa siku | Kulaza Gari kwa siku. |
| Gari ya Mizigo zaidi ya Tani 5 | 1,000/= | 3,000/= | 5,000/= |
| Gari la Mizigo chini ya Tani 5 | 500/= | 2,000/= | 3,000/= |
| Pick up/Station Wagon | 500/= | 2,000/= | 2,000/= |
| Lori lenye Trela zaidi ya tani 3 | 500/= | 2,000/= | 2,000/= |
| Lori lenye Trela tani 3 na zaidi | 500/= | 3,000 /= | 4,000/= |

B. VYOMBO VYA USAFIRI WA ABIRIA

| Na. | Aina ya Chombo | Ushuru(Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Basi Dogo la abiria kati ya 1 – 20 | 1,500/= kwa siku |
| 2. | Basi kubwa la abiria kati ya 20 – 28 | 2,000 /= kwa siku |
| 3. | Basi kubwa la abiria zaidi ya 28 | 3,000/= kwa siku |
| 4. | Gari Dogo (Taxi Cab) | 1,000/= kwa siku |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 1,000/= kwa siku |
| 6. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 1,500/= kwa siku |
| 7. | Pikipiki | 200/= kwa siku |
| 8. | Bajaji | 200/= kwa siku |
| 9. | Magari mengine | 1,000/= kwa siku |
| 10. | Ada ya Kuingia stand kwa mtu mmoja asiye na tiketi | 200/= kila anapoingia |

C. KUVUTA NA KUHIFADHI CHOMBO CHA USAFIRI KILICHOVUNJA SHERIA

| *Na.* | *Aina ya Chombo* | *Gharama za kuvuta* | *Gharama za kuhifadhi kwa siku* |
|---|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria kati ya 20-28 | 150,000/= | 20,000 |
| 2. | Basi kubwa la abiria 28 | 200,000/= | 20,000 |
| 3. | Basi Dogo la abiria kati ya 1-20 | 100,000/= | 20,000 |
| 4. | Gari Dogo (Taxi Cab) | 80,000/= | 20,000 |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 80,000/= | 20,000 |
| 6. | Lori na Trela chini ya tani 3 | 200,000/= | 20,000 |
| 7. | Lori na Trela tani 3 na zaidi | 300,000/= | 20,000 |
| 8. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 80,000/= | 20,000 |
| 9. | Magari mengine | 150,000/= | 20,000 |
| 10. | Pikipiki na Bajaji | 20,000/= | 10,000 |

D. ADA YA USAJILI WA TEKSI, PIKIPIKI NA BAJAJI

| *Na.* | *Aina ya Chombo* | *Ada ya usajili kwa mwaka* |
|---|---|---|
| 1. | Teksi | 10,000 |
| 2. | Pikipiki | 5,000 |
| 3. | Pikipiki ya magurudumu matatu | 5,000 |

VIII. USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Na | Aina ya zao | Ushuru (TShs.) |
|---|---|---|
| 1 | Mbao za miti laini ya kupandwa na saizi aina zote | 5% ya thamani kulinga na bei ya soko . |
| 2 | Mbao za miti ya asili na saizi aina zote | 5% ya thamani kulinga bei ya soko. |
| 3 | Nguzo za miti laini na ngumu (softwood & hardwood) zenye kipenyo kati ya 5cm – 10cm | 5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko. |
| 4 | Nguzo za miti ya laini na ngumu (softwood & hardwood) zenye kipenyo kati ya 10cm – 20cm | 5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko. |
| 5 | Mkaa kwa gunia la kilo 50 | 5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko. |
| 6 | Mkaa kwa gunia la debe 10 | 5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko. |
| 9 | Asali | 5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko. |
| 10 | Mazao mengine yasiyo ya mbao | 5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko. |

IX. ADA YA UPIMAJI WA ARDHI NA VIBALI VYA UJENZI

| Na | *A. Ada ya Kibali cha Ujenzi* | *Kwa kila kibali* |
|---|---|---|
| 1 | Mnara wa simu | 500,000/= |
| 2 | Jengo la Ghorofa moja | 100,000/= kwa kila ghorofa |
| 3 | Nyumba za Biashara | 50,000/= |
| 4 | Nyumba ya Makazi | 20,000/= |
| 5 | Kituo cha mafuta | 250,000/= |
| 6 | Majengo ya Taasisi Binafsi | 150,000/= |
| 7 | Maghala na Bohari. | 100,000/= |
| 8 | Ujenzi wa Uzio | 100/= kwa "Sq meter |
| 9 | Majengo ya Ibada | 100,000/= |
| 10 | Vituo vya Utalii/Mapumziko | 250,000/= |
| 11 | Majengo ya Viwanja | 1,000,000/= |
| 12 | Viwanda Vidogo Vidogo vya Huduma | 200,000/= |
| 13 | Ada ya uchunguzi wa ramani za ujenzi | 10,000/= |
| 14 | Ada ya ukarabati wa nyumba | 15,000/= |

| *Na* | *B. Ada ya mabadiliko ya Matumizi ya Jengo* | *Kwa kibali* |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba ya kuishi na biashara | 40,000/= |
| 2 | Nyumba ya Biashara | 60,000/= |
| 3 | Nyumba ya kuishi | 30,000/= |
| 4 | Ghorofa | 150,000/= |
| 5 | Kiwanda, Bohari, Ghala | 100,000/= |
| 6 | Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Makazi) | 20,000/= |
| 7 | Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Biashara) | 50,000/= |

| Na. | *C. Ada za huduma ya ardhi* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya maombi ya kumilikishwa kiwanja | 20,000/= kwa kila ombi. |
| 2 | Kutambua eneo (Plot identification) | 10,000/= kwa kila plot |
| 3 | Kurudishia mawe yanaonesha mipaka (Beacon replacement) | 6,000/= kwa kila jiwe |
| 4 | Ada ya kukagua ramani | 20,000/= kwa ramani |

X. USHURU WA HOTELI (Hotel Levy)

| <u>*Na.*</u> | <u>*Aina ya Biashara*</u> | <u>*Kiwango*</u> |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kulala wageni | 10% ya mauzo kila chumba kwa siku |

XI. ADA NA USHURU WA HUDUMA NYINGINE

| *Na.* | *Ada* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1 | Gharama ya kuhifadhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura hovyo. | 10,000/= ng'ombe kwa siku<br>5,000/= mbuzi kwa siku<br>5,000/= kondoo kwa siku<br>10,000/= punda kwa siku<br>10,000/= ngamia kwa siku.<br>10,000/= mbwa kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | siku. |
| 2 | Faini ya kutovaa sare kwa wahudumu wa Bar au Mgahawa au Hotel na maeneo mengine ya kutoa huduma za vyakula au vinywaji kwa Umma. | 10,000/= kwa tukio. |
| 3 | Ada ya usajili vikundi vya ujasiliamali | 70,000/= kwa ombi |
| 4 | Ada ya vikundi vya kijamii | 20,000/= kwa ombi |
| 5 | Ada ya kukagua hesabu za shule za Sekondari Binafsi | 100,000/= kwa ombi |
| 6 | Ada ya pango la ardhi kwa wamiliki wa maeneo yaliyopangishwa Minara ya Simu | 5% ya alicholipwa |
| 7 | Mauzo ya vitabu vya stakabadhi za fedha za shule za Serikali za Vijiji. | 7,500/= kwa kitabu. |
| 8 | Mauzo ya Hati za Malipo vijijini. | 7,500/= kwa kitabu |
| 9 | Mauzo ya vitabu vya hati za malipo shule za Msingi na Sekondari | 7,500/= kwa kitabu |
| 10 | Mauzo ya Vitabu vidogo vya Ushuru mbalimbali | 5,000/= kwa kitabu |
| 11 | Ushuru wa kufanya biashara katika eneo la Halmashauri ngazi ya Kata au kijiji. | 500/= kwa siku |
| 13 | Vitabu vya ushuru wa Hotel au nyumba ya kulala wageni | 5,000/= kwa kitabu |
| 14 | Leseni ya Biashara ya Samaki | 20,000/= kwa leseni |

| | | |
|---|---|---|
| 15 | Kibali cha kufanya shughuli za uchimbaji madini | 100,000/=Kwa mwaka |
| 16 | Kibali cha kununua mazao ya biashara | 200,000/=kwa kibali |
| 17 | Ushuru wa uchakataji wa bidhaa au mazao(precessing fee) | |
| | (a) Mchele | 500/= kwa gunia |
| | (b) Mahindi na ngano | 1000/= kwa tani |
| 18 | Kodi ya vibanda kwa watu waliopangisha vyumba vya biashara. | 5% ya kodi ya pango. |

XII. ADA YA MAOMBI YA ZABUNI

| *Na .* | *Ombi* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1 | Zabuni ya ushuru Minada au masoko na mazao | 50,000/= kwa kila ombi |
| 2 | Zabuni ya kutoa huduma na kazi mbalimbali | 50,000/= kwa kila ombi |
| 3 | Zabuni ya kazi za ujenzi. | 100,000/= kwa kila ombi |

XIII. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na | Aina ya Madini | Tani | Kiwango Tsh. |
|---|---|---|---|
| 1 | Mchanga,Kokoto, mawe , kifusi | 1-3½ | 3,000/= kwa kila safari |
| 2 | Mchanga ,Kokoto,mawe,kifusi | 3½ -7 | 5,000/= kwa kila safari |
| 3 | Mchanga,kokoto,mawe, au kifusi | zaidi 7 | 8,000/= kwa kila safari. |
| 4 | Madini ya marumaru | | 20,000/= kwa kila safari |
| 5 | Utengezaji wa tofali kwa kutumia mwamba. | | 20,000/= Kwa safari |

XIV. USHURU WA KUFANYA BIASHARA KATIKA MAGULIO AU MINADA AU MASOKONI.

| Na | Aina Ya Bidhaa | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mitumba | 500/= kwa siku |
| 2 | Vyombo vya nyumbani. | 500/= kwa siku |
| 3 | Nguo za dukani | 500/= kwa siku |
| 4 | Samaki | 500/= kwa siku |
| 5 | Urembo | 500/= kwa siku |
| 6 | Viatu | 500/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Biashara nyinginezo. | 500/= kwa siku. |

XV. USHURU WA KUSHUSHA MIZIGO KATIKA ENEO LA SOKO LOLOTE LILILOTENGWA NA HALMASHAURI

| Na | Aina ya chombo cha usafiri | Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Uzito wa kuanzia tani 1 - 5 | 2,000/= |
| 2 | Uzito wa kuanzia tani 6 – 10 | 5,000/= |
| 3 | Uzito wa kuanzia tani 11 – 20 | 10,000/= |
| 4 | Uzito wa kuanzia tani 20 - 50 | 15,000/= |

JEDWALI LA PILI
(Kimetolewa chini ya kifungu cha 8)
A. KIBALI CHA UJENZI

Form Na……………………..
Kwa: ………………………………………...…………....... ( Jina la mwombaji)

KIBALI HIKI cha ujenzi kimetolewa/kinakataliwa leo hii tarehe…………………mwezi…………………………mwaka……………………kwa MS…………………………………………….wa S.L.P ……………, kwa ajili ya kiwanja Na………Kitalu ………… eneo la ………………Katika eneo la mamlaka ya Halmashauri. Mwombaji ameambatanisha /hakuambatanisha maombi yake ya kibali cha ujenzi na hati au vielelezo vifuatavyo

i. Stakabadhi ya malipo ya ada ya kibali………………….………
………………………………………………………………………..
ii. Stakabadhi ya malipo ya ada ya ukaguzi wa ramani……………
………………………………………………………………………..
iii. Ramani ya majengo:
iv. Nyaraka zozote zinazohusu kiwanja anachotaka kujenga:……..
………………………………………………………………………..
v. Na. ya stakabadhi ya malipo ya ada ya upimaji ………………..
………………………………………………………………………..
vi. Na.ya stakabadhi ya malipo mengine ya Serikali………………
…………………………………………………………………….
vii. Mkataba wa mauzo ya plot (kama upo); ………………………
…………………………………………………………………….

Nakubali/ Nakataa kuwa ramani ya majengo inakidhi / haikidhi masharti ya kiafya au matumizi ya kiwanja na hivyo aendelee/ asitishae ujenzi na kurkebisha ramani..

…………………………………………
Mhandisi Ujenzi /Mkurugenzi

*Futa isiyohusika

B. KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

Kibali kinatolewa kwa……………………………………………..kuchimba, kusambaza au kusafirisha Madini ya ujenzi kutoka eneo la…………………………..kupeleka eneo la…………………………………………kwa ajili ya shughuli ya………………………….kuanzia tarehe………mwezi………..mwaka…………hadi tarehe………mwezi…………mwaka………….kwa masharti yafuatayo:-

1. Mwombaji amelipa Tshs 50,000/= kwa ajili ya kibali cha uchimbaji/usafirishaji wa madini ya Ujenzi.

2. Mwombaji yuko tayari kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi.

……………………………………………
MKURUGENZI MTENDAJI

C. FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO YA CHAKULA/ BIASHARA

FOMU NA. ………….. Tarehe………………….

(Ijazwe na mwombaji)

(SEHEMU A)

1. Jina la Mwombaji …..................................................…………………
2. Jina la Kampuni au Shirika……………………………..……………….
3. Anuani yake S.L.P……………Simu……………….Wilaya……………
4. Mahali Ofisi yake ilipo; Mtaa……………………………………………
   Kata……………………………Wilaya……………………..……………
5. Mahali anapoishi:Mji…………………..……..Mtaa………………………
6. Mahali biashara ilipo…………………………..Mtaa…………..…………
7. Namba ya leseni ya Biashara……………………………………………
8. Namba ya kuandikishwa Shirika, Kampuni ……………………………
9. Maeneo ambayo mnunuzi atanunua mazao chakula au biashara……….
   …………………………………………………………………………...
10. Mazao anayotaka kununua…………………………...…………………
11. Kiasi anachotaka kununua (Kgs)………………………………………
12. Masoko/kijiji atakaponunua……………………………………………………………
13. Maghala yake: Mji……………………….Mtaa………………………Block No………………………….
14. Jina la Ghala/Maghala…………………………………………………..

Nakala ya kibali itunzwe kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote:

Nakala ya kibali hiki itabaki kwa:

1. Mkuu wa Wilaya ya ………………………………………
2. Mkrugenzi Mtendaji(w)……………………………………
3. Afisa Mtendaji wa kijiji cha ………………………………
4. Afisa Mtendaji kata ya ……………………………………

NATHIBITISHA kwamba maelezo yote niliyoyatoa hapo juu ni sahihi na kweli.

i. Jina la Mwombaji……………………………………..
ii. Sahihi ya Mwombaji……………………………………..
iii. Muhuri…………………………………………………….
iv. Tarehe……………………………………………………..

(SEHEMU B)

(Ijazwe na Halmashauri)

15. Mwombaji aliyetajwa hapo juu amepewa/hakupewa kibali cha kununua mazao kwa sababu
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……………………………………

16. Mwombaji amelipa/atalipa ushuru wa Tsh…………………………………kwa kiasi cha mazao atakayonunua kama alivyoyataja hapo Na. 12 hapo juu, yaani kilo……………………………………………………………………….kwa msimu wa ununuzi wa Mwaka……………………….………….
    i. Jina la Afisa……………………….………………………………
    ii. Sahihi……………………………….……...……………………..
    iii. Cheo………………………………………..…………………..
    iv. Tarehe……………………………………….……………………
    v. Muhuri……………………………………..…………………...

………………………………………

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya

JEDWALI LA TATU

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 13)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Mbeya..., kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya Mbeya za Mwaka 2019.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……....……. ya Mwezi……......…… Mwaka ………………….

*Jina*……………………………….. *Saini*…………………………………….

N

Mbele ya :

Jina: ……………………………………………

Cheo: ……………………………..…………

Saini: ……………...……………………………

Likiri na Mhuri wa Halmashauri ya wilaya ya mbeya umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kilichofanyika tarehe …… mwezi….mwaka…..mbele ya:-

STEPHEN E. KATEMBA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Mbeya*

MWALINGO MWAYONGO KISEMBA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Mbeya*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
27Agost 2018

SELEMANI S.JAFO ( MB)
*Waziri wa Nchi-or Tamisemi*